TANGAZO LA SERIKALI NA. 5 Limetolewa tarehe 4/1/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA. NA 272)

# AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu Na.28 (d))*

AMRI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MTWARA ("MTWARA WSSA") (YA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018

Kichwa cha Amri

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mtwara ("Mtwara WSSA")(ya Kurekebisha Bei za Huduma za Majisafi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2018.

Tarehe ya kuanza

2. Amri hii itaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Januari 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mtwara WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo-

(a) ifikapo tarehe 31 Machi 2019 au kabla, Mtwara WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara wa kipindi cha mwaka 2018/19 hadi 2020/21 uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa, na mpango kazi wa utekelezaji wa masharti ya Amri hii. Pia, Mpango Biashara

uhusishe miradi itakayotekelezwa kwa mwaka 2020/21 yenye thamani ya shilingi 1,090 milioni;

(b) Mtwara WSSA itahakikisha itaendelea kuwasilisha taarifa zake za fedha zilizokaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) au mtu yeyote aliyeidhinishwa kutokana na kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kuhakikisha inawasilisha EWURA rasimu za mahesabu yaliyokaguliwa;

(c) ifikapo tarehe 30 Juni 2019 au kabla, Mtwara WSSA itafanya tathmini ya thamani ya mali zake na kuwasilisha EWURA taarifa ya tathmini iliyothibitishwa na Mtathmini aliyesajiliwa;

(d) Mtwara WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa;

(e) Mtwara WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mtwara WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mtwara WSSA katika siku zijazo;

(f) Mtwara WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Amri hii pamoja na miradi itakayoidhinishwa na EWURA

kwa mwaka 2020/21 na itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Amri hii.

Kutenguliwa kwa Amri

5. Amri hii inatengua matumizi ya Amri Na. 2015-005 ya tarehe 1 Juni 2015 katika maeneo yanayohudumiwa na Mtwara WSSA.

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

_____________

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi ya Maji kwa Uniti | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0 - 10 | 945 | 1,200 | 1,300 | 1,090 | 1,110 | 1,110 |
| | >10 - 20 | 1,090 | 1,300 | 1,400 | 1,260 | 1,280 | 1,280 |
| | >20 | 1,190 | 1,350 | 1,450 | 1,370 | 1,400 | 1,400 |
| Biashara | 0 - 10 | 1,735 | 2,600 | 2,700 | 2,000 | 2,030 | 2,030 |
| | >10 - 20 | 1,885 | 2,700 | 2,800 | 2,170 | 2,210 | 2,210 |
| | >20 | 2,080 | 2,750 | 2,850 | 2,400 | 2,440 | 2,440 |
| Taasisi | 0 - 10 | 1,735 | 2,600 | 2,700 | 2,000 | 2,030 | 2,030 |
| | >10 - 20 | 1,835 | 2,750 | 2,850 | 2,110 | 2,150 | 2,150 |
| | >20 | 2,030 | 2,800 | 2,900 | 2,340 | 2, 380 | 2,380 |
| Viwandani | 0 - 10 | 1,735 | 2,600 | 2,700 | 2,000 | 2,030 | 2,030 |
| | >10 - 20 | 1,835 | 2,700 | 2,800 | 2,170 | 2,210 | 2,210 |
| | >20 | 2,080 | 2,800 | 2,900 | 2,400 | 2,440 | 2,440 |
| Magati | | 1,000 | 1,500 | 1,500 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| Majaba | | 3,000 | 3,600 | 3,600 | 3,450 | 3,510 | 3,510 |
| WAT | | 1,266 | | | 1,460 | 1,480 | 1,480 |

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

| Kundi la Wateja | Bei za Sasa | Tozo zilizopendekezwa | | Tozo zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/2020 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 2000 | - | - | - | | |
| Commercial | 5000 | - | - | | | |
| Institution | 5000 | - | - | | | |
| Industrial | 6000 | | - | | | |

Jedwali Namba 1(c): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | Asilimia ishirini ya gharama za maunganisho kama inavyojieleza katika sehemu ya 24 ya Kanuni za Maji za mwaka 2013 | | |
| Biashara | | | | |
| Taasisi | | | | |
| Viwanda | | | | |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa, Iliyopendekezwa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada zilizopendekezwa | | Ada zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/2020 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Domestic | 20000 | 25,000 | 25,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Commercial | 30000 | 40,000 | 40,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Institution | 30000 | 40,000 | 40,000 | 30,000 | 30,000 | 30,000 |
| Industrial | 40000 | 50,000 | 50,000 | 40,000 | 40,000 | 30,000 |

---

JEDWALI LA PILI

---

MIRADI ITAKAYOTEKELEZWA KWA KUTUMIA FEDHA ZITOKANANZO NA MAUZO YA MAJI

| Maelezo ya Kazi Zitakazotekelezwa | Shilingi (milioni) | |
|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 |
| Matengenezo ya kusambaza maji katika eneo la Mbuo/Mkunwa | 250 | 0 |
| Kusambaza maji eneo la Mbabawala Chini | 250 | 250 |
| Matangenezo ya Majengo ya Ofisi na Mitambo | 35 | 30 |
| Kubadilisha Pampu ya Kisima Na. 6 (B/H 6) | 10 | 10 |
| Kurekebisha mfumo wa kufikisha maji na Pampu kuu ya kusukuma maji eneo la Mtawanya na Mikindani | 10 | 10 |
| Kutengeneza Pampu za Usambazaji maji Mtwara + Mikindani | 50 | 50 |
| Kutengeneza Valvu na Chemba katika mabomba ya kusafirisha maji | 50 | 50 |
| Kufanya marekebisho katika Matenki ya maji yaliyopo | 10 | 10 |

| Maelezo ya Kazi Zitakazotekelezwa | Shilingi (milioni) | |
|---|---|---|
| | 2018/19 | 2019/20 |
| Kufanya matengenezo ya Magati 46 yaliyopo kwa sasa | 10 | 10 |
| Jumla Ndogo (Kubadilisha) | 675 | 420 |
| Kuongeza Uzalishaji wa maji kutoka Uzalishaji wa sasa wa Mita za Ujazo 9000 hadi 15,000 kwa Siku. | 250 | 200 |
| Kuongeza Mtandao wa maji (Mbae Masharikirk, Mtepwezi, Lilungu, Mitengo Chipuputa) | 360 | 320 |
| Kununua Vitendea Kazi kupunguza upotevu wa maji kutoka asilimia 30 ya sasa hadi asilimia 25 ifikapo 2020 | 100 | 100 |
| Kujenga nyumba za makazi eneo la Mangamba na Mtawanya | 50 | 50 |
| Jumla Ndogo - (miradi mipya) | 760 | 670 |
| Jumla ya Gharama za Miradi | 1,435 | 1,090 |

## JEDWALI LA TATU

### VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2019/20)

| Maelezo | Kipimo | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa maji safi | No. | 1058 | 1100 | 1100 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 27 | 25 | 25 |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Asilimia ya Idadi ya watu wanaoishi kwenye eneo lenye mtandao wa maji safi | % | 92 | 95 | 97 |
| Asilimia ya idadi ya watu wanaohudumiwa na Mtwara WSSA | % | 80 | 90 | 92 |
| Wastani wa muda wa huduma | % | 13 | 15 | 16 |
| Kiwango cha idadi ya maunganisho ukilinganisha na idadi ya nyumba zote | % | 60 | 75 | 75 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji mapato | % | 85 | 95 | 95 |

Dodoma,
.........................., 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*